# CLASS 8 MID TERM 3 2021
# KISWAHILI

***Soma kifungu kifuatacho, king nafasi 1 mpaka 15 kwa kila nafasi umepewa viteuzi vinne.***

***Chagua kilicho sahihi zaidi***

Tamaa ___1___ ni ya ___2___ kukamia ___3___ na pato nono ___4___ kujenga vipango ___5___ kujipatia hongo.

Wachanganuzi ___6___ masuala ya ___7___ wanaliona ___8___ kuwa njia ___9___ kuhinikiza ___10___ na kuridhia mapato ___11___.

Wanadai kuwa wengi ___12___ viongozi wa kidini wanawajazibisha ___13___ wao wakatolea ya kuwapa utajiri ___14___ wao wakasalia wasiokuwa na mbele ___15___ nyuma. Je, wanawadhihirisha kuwa wajinga ndo waliwao?

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | hiki | hizi | yenye | hii |
| 2. | kuwainua | kujiinua | kuyainua | kumwinua |
| 3. | beberu | mbeberu | mbeleko | mbeko |
| 4. | mbali na | mbali kwa | mbali ya | mbali pa |
| 5. | kwa | ya | vya | za |
| 6. | wenye | wa | na | kwa |
| 7. | utaifa | taifa | kitaifa | ulimwengu |
| 8. | hii | lote | lenye | hili |
| 9. | ja | ya | la | kwa |
| 10. | halali | chai | ukarimu | ufisadi |
| 11. | haramu | uwajibikaji | uhalali | kujukumika |
| 12. | miongoni mwa | kati ya | nyuma ya | baadhi ya |
| 13. | mashabiki | wadhamini | mfuasi | wafuasi |
| 14. | huku | kule | shufaa | kumbe |
| 15. | bali | kefu | wala | japo |

**Jibu kulingana na maagizo kutoka swali la 16-30**

16. Andika sentensi kwa wingi. Ujukuti wa mnazi umekauka.
A. Jukuti ya mnazi zimekaukaa
B. Ujukuti wa minazi umekauka
C. Njukuti za minazi zimekauka
D. Majukuti ya nazi yamekauka

17. Chagua kivumishi katika sentensi Jumba jingine lilibomolewa jana jioni
A. jana B. jingine
C. jioni D. lilibomolewa

18. Nilimsaidia alipokuwa akiumwa Kiambishi Ni kimetumikaje katika sentensi
A. Kuonyesha wakati
B. Kiwakilishi nafsi
C. Kielezi
D. Kuonyesha uhusiano wa nomino na mahali

19. Tambua maanaya sentensi Nisingalikuja nisingalimpata darasani
A. Alimpata darasani kwa sababu alienda
B. Hakuenda wala kumpata darasani
C. Alienda lakini hakumpata darasani
D. Licha ya kuenda hakumpata darasani

20. Tambua matumizi ya "karibu" Alianguka karibu afe.
A. masafa
B. kuonyesha makaribisho
C. karibu ya kiasi
D. nusura

21. Chagua jibu sahihi.
Cheichei _______________
A. hewala B. cheichei
C. ewa D. binuru

22. Chagua nomino kutokana na kitenzi kula
A. laza B. kula
C. mlo D.mlaji

23. Wakati wa baridi kali na upepo bila mvua huitwa?
A. mchoo B. kiangazi
C. vuli D. kipupwe

24. Vazi linalovaliwajuu ya nguo kwa mbele ili kukinga nguo zisichafuke huitwa
A. kizibao B. kimori
C. joho D. kanga

25. Chagua kundi la vimelea
A. Papasi, kitumbi, tekenya
B. Kichocho, kifaduro, pepopunda
C. Utitiri. chozi, tongo
D. Kima, sisimizi. bundi

26. Geuza sentensi katika usemi wa taarifa
" Ukitia bidii utafaulu mtihani mwalimu alimshauri mwanafunzi
A. Mwalimu alimshauri mwanafunzi kuwaakitia bidii atafaulumtihani
B. Mwalimu alimshauri mwanafunzi, ukutia bidii utafaulu
C. Mwalimu alimshauri mwanafunzi kuwaangetii bidii angefaulu mtihani
D. Mwanafunzi alimshauri mwalimu kuwa angetia bidii angefaulu mtihani

27. Tegua kitendawili Siri ya kaburi aijuaye ni:
A. kifo B. maiti
C. sanduku D. kaburi

28. Andika sentensi katika ukubwa na wingi: Ndege wa mto hunywa maji safi
A. Madege wa majito yanywa maji safi
B. Madege ya mito yanywa maji masafi
C. Dege ya mito hunywa maji safi
D. Mandege ya mito yanywa maji masafi

29. Kanusha sentensi: Ningesoma ningefaulu mtihani
A. Nisingesomanisingefaulu mtihani
B. Nisingalisoma nisingefaulu mtihani
C. Nisingalisoma ningefaulu mtihani
D. Nisingesoma nisingefaulu mtihani

30. Tajiri aliketi mkabala wa sultan. Kifua cha sultan kilitazamakusini mashariki. Je, kisogo cha tajiri kilitazama wapi?
A. Kaskazini magharibi
B. Kaskazini mashariki
C. Kusini mashariki
D. Kusini magharibi

***Soma taarifa ifuatayo kisha uiibu maswali 31 - 40***

Utalii nchini ni wa hali yajuu. Tunapata watalii wengi kutoka uingereza, marekani, ijapani na kwingineko. Huzuru nchi yetu kujionea wanyama katika mbuga zetu. Amboseli, Tsavo mashariki na Magharibi ni baadhi ya mbuga zinazopata watalii wengi humu nchini. Majumba ya ukumbusho kama vile makavazi ya Nairobi na Fort Jesus hutukumbusha kuhusuhi historia mbalimbali. Si mavazi, si ala, si majengo, si desturi natamaduniorodha haiishi. Watalii hupendelea pia kupunga hewa sehemu za pwani na huogelea kwenye Bahari Hindi. Mandhari ya maeneo ya mwambao huvutia mno. Hata kule kujilaza tu kwenye ufuo wa bahari hasa mchangani. Kutokana na shughuli za utalii, tunapata manufaa belele. Tunapata pesa za kigeni ambazo hutusaidia katika miradi ya kujenga hospitali, barabara, shule na kadhalika. Wengi wetu hupata gange kama madereva, wahudumu, mataarishi, wapishi na wengine wengi.

Watalii wengi huwamezea mate wanyama wetu, ambao hupatikana katika makazi yao maalumu, majini, mitini, pangoni na savanna kwajumla. Si ajabu kuona tumbili wakichupakutoka mti mmoja hadi mwingine, au simba mawindoni akifuata swara unyounyo.

Yote yang'aayo si dhahabu. Maingiliano yetu na wageni yana madhara mbalimbali. Vijana wetu huathiriwa kwa kuiga tabia na mienendo isiyofaa. Uraibu wa mihandarati, mavazi yasioambatana na tamaduni zetu ni baadhi tu ya mambo yasiyotufaa. Watoto wa shule hutoroka shuleni kujipatia kazi za kijungu jiko kama vile kuwabebea watalii virago vyao na kuwatembeza mitaani. Wengine wamesahau mwacha mila ni mtumwa. Wamesahau mila zetu na kuiga zile za kigeniNi wajibu wa serikali kuwaelimisha wananchi wote ili tusibeze tamaduni zetu. Tukumbuke elimu ndiyo ngao

31. Ni mambo gani tunayojifunza katika makavazi nchini
   A. Mbuga za wanyama,savanna na majengo
   B. Wanyama wa savanna, pangoni na majini
   C. Mavazi aina mbalimbali, majengo, desturi tamaduni na kadhalika
   D. Mavazi na wanyama pori

32. Kutalii ni
   A. kuranda mbali na nyumbani
   B. kuzuru, kuona na kujifunza mageni
   C. kuzuru savanna
   D. kuzuru wanyama

33. Yanayowavutia watalii wengi nchini ni?
   A. Tamaduni za nchini
   B. Wanyama wa pori katika makazi yao
   C. Simba mawindoni
   D. Ufuo wa bahari unapootajua

34. Eleza sentensi iliyo sahihi kulingana na taarifa hii
   A. Utalii una madhara pekee ukomeshwe
   B. Watalii hutoa watoto shuleni ili kuwabebea mizigo
   C. Utalii umeenea mwambao pekee
   D. Tuaiige mila za kigeni na kusahau zetu

35. Ni jambo lipi la muhimu tunalolipata kutokana na utalii
   A. Kazi mbalimbali
   B. Tamadhuni na tabia zao
   C. Kazi na kijungu jiko
   D. Pesa za kigeni

36. Yote yang'aayo si dhahabu ni methali iliyotumika kuelezea?
   A. Tujihadhari na mambo tunayoyapata kutoka nchi za kigeni yasitudhuru
   B. Yote tunayoyapata ni kama dhahabu.
   C. Yote tunayoyapata tuyapokee yalivyo
   D. Mambo yote ya nchi za kigeni ni mabaya

37. Serikali imetahadharishwa kufanya nini kuondoa madhara ya utalii
A. Kupata elimu ili kupatakazi za maana
B. Kupata elimu kuimarisha utalii nchini
C. Kupata elimu kuelewa umuhimu wa tamaduni zetu
D. Kupata elimu kuangalia watalii

38. Madhara yapatikanayo kutokana na utalii ni?
A. Kuua wanyama, uraibu, kutoroka shule
B. Utamaduni kuzorota kwa kutumia pesa za kigeni
C. Pesa za kigeni, kazi za kijungu jiko na kutoroka shule
D. Uraibu, mavazi yasiyofaa, kutoroka shule na kadhalika

39. Kuchupa kutoka mti rnmoja hadi mwingine ina maana gani?
A. Kurukaruka waonapo watalii
B. Kurukaruka kutoka mti rnmoja hadi mwingine
C. Kuchupa mtini hadi mwingine
D. Kurukaruka kutoka mti rnmoja hadi mwingine

40. Kazi ya kijungu jiko ni
A. Kazizenye mishahara minono
B. Kazi zinazowasaidia watoto shuleni
C. Kazi zakujitamtiariziki tu
D. Kazi zenye manufaa makubwa kwao

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali kutoka 41- 50**

Ni jambo ambalo ni bayana kwamba, ulialifu unazidi kukita mizizi katika pembe zote ulimwenguni. Walimwengu wamejipata hali taabani. Kila kukicha, wanakumbwa na tisho maishani mwao. Tisho hili halitoki kwa wanyama. Kamwe, ulimwengu si mahali salama tena pa kuishi. Baadhi ya binadamu wamegeuka kuwa hayawani. Kuanzia vijijini hadi mijini. Wapo wanyama tumbi nzima kwenye ngozi na rangi za binadamu. Hata wanazo lebasi za binadamu. Kila wakati tunatangamana na wao

Ama kweli, **uhalifu umekulula mipaka**. Hali imefika kiwango kwamba hata maeneo mengine yametajwa kuwa hatari kwa binadamu. Ipo baadhi ya mji ambayo inasemekana kuwa dakika haipiti bila kitendo cha uhalifu kutokea.

Wizi wa mabavu umezidi, ugandamizaji wa kila aina umeenea na kuzagaa. Ubakaji hata kwa watoto limekuwa jambo la kawaida katika baadhi ya maeneo. Eneo la kusini mwa Afrika limekuwa katika vyombo vya habari kuhusiana na uovu huu.

Unafiki, usaliti, ushutumiaiaji na ufisadi ni maovu ambayo yanatisha kuangamiza jamaa nzima. Imekuwa nadra ndugu kuaminiana, bibi na mume kuaminiana. Shtuka kikwenu nikikwambia kuwa nimewaona wazazi na watoto wao ambao hawapikiki katika chungu kimoja. Mola mwema tusaidie. Waumini wana shaka kuwahusu baadhi ya wachungaji wao. Ni nani asiyeshangaa asikiapo ndugu wa toka nitoke wakichanjana kama kuni? Nani mwenye utu kati ya wachache waliobaki asiyebung'aaa aikiapo mume au mke wa ndoa akimchimbia mwenzake kisima? Nani asiyeatika moyo asikiapo mchungaji akiwatapeli wanakondoo wake? Na kwambia hawa ni wale waliotabiriwa. Wanawachinja kondoo walionona. Mungu wangu, ulimwengu unaelekea wapi?

Je, nini kiini cha maovu haya yote? Wapi tulipoenda mrama? Wapi tulipoteleza na inaelekea hata kuanguka? Tetesi na maoni mengi yametolewa. wengi wanasema ni utabiri umetimia, lisemwalo lipo na kama halipo lisubiri li njiani.

Lawama na shutuma zimetupiwa makundi mbalimbali. Wavyele, hatujaepuka kuelekeza kidole. Wazazi, inasemekana wamechangia pakubwa kuifanya dunia kurudi kuwa mahali hatari kuishi.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

Wamepuuza wajibu na jukumu lao la kuwaongoza na kuwaelekeza wana wao. Wamekosa kuwa vielekezo vyema kwa mabin na mabinti wao.

Iwapo wazazi wamevalia jukumu lao miwani, basi wa kuwaongoza watoto ni nani na ilhali tunajua kuwa mwana hutazama kisogo cha nina?.

Kuzorota na kudorora kwa uchumi vilevile kunasemekana kuwa kumechangia si haba. Watu wengi wamejipata bila **kazi wala bazi**. Hawana njia yoyote halali ya kuzumbua riziki. Kimbilio lao ni wapi? Wengi hupata kimbilio katika ulimwengu wa uharibifu. Vijana wetu wanaingilia uhalifu wa kila aina na baadhi yao huvamia mwengine kama vile usherati na ulawiti. Waitwao baba na mama sukari. Wanazidi kuwawekea vijana wetu **chambo**.

Hali mbaya ya uchumi pia inasemekana kuchangia katika utumishi wa mihadarati. Vijana wetu wanapokosa ajira, wanapoteza matumaini katika hali hiyo wanastahili mtu waku waliwaza. kwa bahati mbaya, mara nyingi hujipata mikononi mwa wahuni na maangamizi. Biwi la dawa za kulevya.

Inaafa sote tushirikane. Tupige darubini tuone ni wapi **tulipoenda tege**. Wakati wa kulaumiana na kushutumiana umepita. Tumelauminiana kwa siku nyingi bila kupata lolote la maana. Wakati ni sasa wa kuchukua hatua **tistsi** la sivyo

41. Kwa mujibu wa msimulizi, ni jambo lipi ambalo ni wazi?
   A. Uovu umedidimia
   B. Usalama umetishiwa
   C. Uhalifu umepungua
   D. Usalama umeimarika
42. Kwa nini wavyele wanalaumiwa?
   A. Hawatoi nasaha vilivyo kwa watoto wao
   B. Wamekosea pesa ya kuwalea watoto
   C. Wameingilia uhalifu
   D. Hawawapendi wana wao
43. Ni wahusika wapi wanaolaumiwa kuwa watapeli?
   A. Wachungaji
   B. Wabakaji na malaya
   C. Akina mama na baba sukari
   D. Majangili
44. Kipi hasa ndicho kiini cha vijana kuingilia uhalifu
   A. Malezi mabaya
   B. Uhayawani
   C. Utumishi wa dawa za kulevya
   D. Umasikini
45. Kwa nini kila kukicha tisho kwa binadamu linazidi?
   A. Kumekuwa na njaa
   B. Umaskini umezidi
   C. Watu wengi wamezidi kupotoka
   D. Wanyama wamezidi kuwavamia binadamu
46. Kulingana na makala wachungaji ni kina nani?
   A. Watu wanaochunga raia wasifanye uhalifu
   B. Wafugaji wanaochunga kondoo
   C. Watu waliotabiriwa
   D. Viongozi wa madhebehu
47. Ni kweli kusema:
   A. Wakati wa kulaumiana ni sasa
   B. Kulaumiana na kushutumiana kumepita
   C. Lawama zimepunguza shida duniani
   D. Tusipojihadhari, maovu yatazidi
48. Eneo la kusini mwa Afika linakumbwa zaidi na uovu gani?
   A. Ubakaji B. Ushirikina
   C. Umalaya D. Ujambazi
49. Kulingana na msemo huu **uhalifu umekulala mipaka** inamanisha
   A. kupita zaidi
   B. kupita kidogo
   C. wizi
   D. ouvu
50. Kwa mujibu wa musimulizi, jukumu kubwa la wazazi ni
   A. kuwaelimisha watoto
   B. kuwafundisha watoto tabia mzuri
   C. kuwapa watoto zawadi
   D. kuoata watoto